**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA PILI

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE

**29 JANUARI, 2016**

**MKUTANO WA PILI - YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE**

**TAREHE 29 JANUARI, 2016**

## I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Naibu Spika) alisoma Dua na kuliongoza Bunge.

**MAKATIBU MEZANI:**
1. Ndg. Lina Kitasi
2. Ndg. Joshua Chamwela

## II. HATI ZA KUWASILIOSHA MEZANI:

Hati zifuatazi ziliwasilishwa mezani:-

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**
Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2015

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mpango wa pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kinachoanzia 2016/17 – 2020/21.

**MWENYEKITI WA KAMATIA YABAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu tathimini ya utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano 2011/12 – 2015/16, pamoja na mapendekezo ya Muundo wa Mpango wa pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano 2016/17 – 2020/ 21.

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARAYA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango juu ya Mpango wa wa pili wa Mendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano 2016/17 - 2020/21.

## III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Wabunge:-

**1. OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na. 38: Mhe. Anna Richard Lupembe

Swali la nyongeza: Mhe. Anna Richard Lupembe
Mhe. Katani Ahmed Katani

Swali la Na: 39: Mhe. Simoni Sebastiani Kapufi

Swali la nyongeza: Mhe. Simoni Sebastian Kapufi
Mhe. Agnes Mathew Marwa

Swali Na. 40: Mhe. Munde Tambwe Abdallah

Swali la nyongeza Mhe. Munde Tambwe Abdallah
Mhe. Devotha Mathew Minja

Swali Na. 41: Mhe. Tunza Issa Malapo

Swali la nyongeza: Mhe. Tunza Issa Malapo

**2. OFISI YA RAISI (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Swali Na. 42: Mhe. Kasuku Samson Bilago

Swali la nyongeza Mhe. Kasuku Samson Bilago

Mhe. Joseph Joman Selasini
Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga

**3. WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na. 43: Mhe. Desderius John Mipata

Swali la nyongeza: Mhe. Desderius John Mipata
Mhe. Boniphace Mwita Getere

Swali Na. 44: Mhe. Abdallah ali Mtolea

Swali la nyongeza: Mhe. Abdallaha Ali Mtolea
Mhe. Marwa Ryoba Chacha

**4. WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Swali Na: 45: Mhe. Kangi Alphaxard Lugola

Swali la nyongeza: Mhe. Kangi Alphaxard Lugola
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia

Swali Na. 46: Mhe. Hamidu Hassani Bobali

Swali la nyongeza Mhe. Hamidu Hassani Bobali

Mhe. Richard Mganga Ndassa
Mhe. Zitto Zuberi Kabwe

**MATANGAZO:**

- Wabunge wanawake wakutane saa 9:00 alasiri katika ukumbi wa Piusi Msekwa;
- Kamati ya Masuala ya Ukimwi ikutane saa 7: 00 Mchana HAZINA;
- Huduma ya utoaji wa Passport kwa Wabunge itaanza kutolewa leo mchana hadi tarehe 2/2/2016;
- Bunge sports Club itatangaza uwepo wa mashindano ya riadha na michezo ya kirafiki wakati wa mapumziko ya wikiend;
- Taasisi ya uwekezaji (UTT) inawakaribisha wabunghe kuona maeneo ya uwekezaji, Hisa na viwanja vya Biashara.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Philip Isdor Mpango alitoa maelezo na kutoa Hoja kwamba Bunge lilijadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kinachoanzia 2016/17 – 2020/21.

**MWONGOZO WA SPIKA**

Wabunge wafuatao walisimama kuomba muongozo:-

1. Mhe. Saed Ahmed Kubenea - alitumia kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kuwa siku ya juzi wakati askari polisi wakiingia Ukumbini na kuwatoa baadhi ya Wabunge nje ya Ukumbi, Wabunge wanawake walidhalilishwa.

- Kiti kilitoa mwongozo kuwa Mbunge asome Kanuni vizuri kuhusu maneno ya Kanuni kuhusiaa na na jambo lililotokea mapema.

2. Mhe. Jesca David Kishoa – alitumia kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kuwa hivi karibuni TAKUKURU ilitangaza kuwapeleka mahakamani Mafisadi wakubwa Je, kwa nini fisadi mhusika wa Escrow (SETTY) hachukuliwi hatua.

- Kiti kilitoa uamuzi kuwa mwongozo huo upo nje ya kanuni.

3. Mhe. James Kinyasi Millya – aliomba mwongozo kuwa wakati swali la Mhe. Kangi Alphaxard Lugola likijibiwa kiti kilimkataza Mbunge asitaje majina ya watu wakati kanuni ya 40(h) inaruhusu majina kutajwa kama ni lazima.

- Kiti kilitoa uamuzi kuwa uamuzi wa Kiti ulishatoka na ni wa mwisho, Mbunge ambaye hajaridhika atumie kanuni kuwasilisha malalamiko yake.

4. Mhe. Zitto Zuberi Kabwe – aliomba mwongozo kuwa Hoja iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango leo inahusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wakati yeye Mwenyekiti ametoa Maelezo yanayohusu Kamati ya Mipango ambapo Bunge hujadili Mpango wa mwaka mmoja tu, Je, huku siyo kuwahisha Shughuli na kwa kuwa Mpango wenyewe wa miaka Mitano haupo si vyema Kanuni ya 68(5) itumike ili kamati ya Kanuni ijadili suala hilo na kutoa ushauri.

- Kiti kilitoa mwongozo kuwa kinalichukua suala hiulo na kitatoa maamuzi baadae.

5. Mhe. Tundu Anthipas Lissu – aliomba mwongozo na kusema kwamba Orodha ya Shughuli za leo inaonyesha kwamba Waziri wa Fedha na Mipango atawasilisha Mpango wa Pili wa Maendeleo na kwa kuwa Mpango huo haupo na pia Muswada wa Mpango huo haupo je, Bunge sasa linajadili kitu gani.

- Kiti kilitoa maelezo kuwa mwongozo huo unalingana na mwongozo ulioombwa na Mhe. Zitto Kabwe na maelezo kuhusu miongozo hiyo yatatolewa baadae.

**HOJA ZA SERRIKALI: (ILIENDELEA)**

- Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia - Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti alisoma Taarifa ya Kamati kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka Mitano;

- Mhe. David Ernest Silinde – Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango alisimama na kueleza kuwa kutokana na utaratibu wa uwasilishwaji

wa Hoja hiyo kuvunjwa, Kambi ya Upinzani haipo tayari kutoa maoni yake kuhusu Mpango huo;

- Kutokana na sababu hiyo na mkanganyiko uliotokea wakati wa miongozo ya Mhe. Zitto Kabwe na Tundu Lissu, Mwenyekiti aliamua kusitisha Shughuli za Bunge ili kupata fursa ya kuliweka vizuri suala hilo la uwasilishaji wa Mpango wa miaka Mitano.

## V. KUSITISHA BUNGE

Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Andrew John Chenge alisitisha Bunge saa 6:30 mchana hadi saa 10:00 jioni.

## VI. BUNGE KUREJEA:

Saa 10:00 jioni Bunge lilirejea na kuongozwa na Mwenyekiti wa Bunge, Mhe. Andrew John Chenge.

- Baada ya kurejea Mwenyekiti alianza kwa kutoa maelezo juu ya miongozo iliyoombwa na Mhe. Zitto Kabwe Zuberi pamoja na Mhe. Tundu Lissu kuhusu Bunge kuvunja Ibara ya 63(3) (c) ya katiba katika kujadili Mpango wa miaka Mitano wa Maendeleo kama Bunge badala ya Bunge kukaa Kamati ya Mipango;

- Mwenyekiti alishauri Serikali kupitia kanuni ya 58(5) iondoe Hoja hiyo na Bunge likubali kuondoa Hoja hiyo ili baade ije kwa njia ya Kamati ya Mipango;

- Mwenyekiti alimwita Mtoa Hoja, Waziri wa Fedha na Mipango ili aombe Idhini ya Bunge kuondoa Hoja hiyo, na baada ya Hoja hiyo kuungwa mkono Bunge lilihojiwa na kuafiki suala hilo.

## VII. KUAHIRISHA BUNGE:

Mwenyekiti aliahirisha Bunge saa 10:30 jioni hadi siku ya Jumatatu tarehe 1/2/2016 saa 3:00 asubuhi.

**DODOMA**
**29 JANUARI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**